TANGAZO LA SERIKALI NA……. LA MWAKA ……

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MANISPAA)
(SURA YA 288), 2002

_____

SHERIA NDOGO

_____

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 89)

_____

SHERIA NDOGO YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA (UDHIBITI NA USIMAMIZI WA RASILIMALI YA UVUVI KWENYE MIALO (BMU)) ZA MWAKA 2017

Jina eneo la matumizi

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama sheria ndogo za Halmashauri ya Manispaa ya Musoma za mwaka 2017 na zitatumika katika eneo lote la Halmashauri.

2. Sheria hizi zitatumika mara baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelekezwa vinginevyo.

"Afisa Muidhinishaji" maana yake ni Afisa yeyote atakayeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia sheria ndogo hizi.
"BMU" maana yake ni Beach Management Unit (kikundi cha usimamizi wa rasilimali za uvuvi kwenye ziwa Viktoria..
"Chombo cha usafiri majini maana yake mtumbwi wa injini au kasi.

"Nyavu" maana yake ni nyavu za makila (gillnets) zenye macho yenye ukubwa wa nchi 5,6 na kuendelea au mm 8.
"Ndoano" maana yake ni ndoano za saizi na 7, 8, 9 na 10 tu zinazoruhusiwa.

"Zana za uvuvi" maana yake ni nyavu, ndoano, karabai na kasha, kasia, injini na mtumbwi.
"Josho" maana yake ni tanga au kipande cha kitambaa kinachofungwa kwenye mtumbwi na kujaza upepo ili kusaidia mtumbwi kutembea majini bila kutumia makasia au injini.

"Kasia" maana yake ni kifaa aina ya mwiko mkubwa kinachotengenezwa kwa kutumia mti au ubao kwa ajili ya kuendesha mtumbwi majini.

4. Ni marufuku mtu yeyote kuingiza chakula cha aina yeyote, pombe ya aina yoyote, matunda ya aina yoyote, kucheza karata za kamari, kulia au kunywea kilevi cha aina yoyote ndani ya uzio.

5. Ni marufuku kutupa vifuniko vya soda au maji, maganda ya miwa, ndizi maeneo ya mwalo.

Uhakiki wa ubora wa Samaki

6. Kamati ya ulinzi wa rasilimali ya uvuvi kwa kushirikiana na Kamati ya Mazingira ndiyo pekee itakayotenga maeneo ya kutoa huduma ya aina yeyote katika eneo la mwalo.

7. Ni marufuku kwa mtu yeyote kufanya biashara ya aina yeyote ile karibu na eneo la kupaki / kuegesha mitumbwi ya uvuvi, shughuli zote za kibiashara zifanyike umbali wa mita ishirini (20) nje kabisa ya mwalo.

8. Mitumbwi yote ya kukusanyia samaki au kusafirisha mizigo au abiria itaengeshwa umbali wa mita 10 (kumi) kutoka kwenye uzio

9. Ni marufuku mtu yeyote kuweka samaki chini au juu ya paa la tishari, darajani au juu ya gari kwenye mchanga

10. Ni marufuku mtu yeyote kukaa juu ya bomba za daraja au tishari kwenye nguzo au mabini ya kuhifadhia samaki trey na vyombo vingine vinavyotumika kupimia au kuwekea samaki, barafu na maji.

11. Ni marufuku mtu yeyote kuingia ndani ya uzio kwenye daraja au tishari bila ruhusa na bila kuwa na kazi ya kufanya.

12. Ni lazima kila mvuvi au mwanachama wa BMU kuhudhuria vikao vya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wavuvi au Kamati ya Mazingira pale vikao vitakapoitishwa na Kamati hizo.

13. Ni marufuku kwa mtu yeyote kujisaidia ovyo eneo la mwalo, katika maji, ziwa Tishari, ghatini au katika mazingira yeyote ya mwalo na barabara.

14. Ni marufuku mtu yeyote kutupa takataka au uchafuwa aina yeyote eneo lolote la mwalo, uchafu utatupwa katika sehemu zitakazotengwa kwa utaratibu wa uongozi wa BMU.

15. Ni marufuku kwa mtu yeyote kuoga, kufua nguo, kuosha vyombo na kunawa kwa kutumia sabuni katika eneo la maji ya mwalo umbali wa mita 200 kulia au kushoto kwa Tishari au Uzio.

16. Kutakuwa na vyoo vya umma vitakavyojengwa na kusimamiwa na Halmashauri katika maeneo ya mwalo na vitaendeshwa kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na sheria za Afya.

17. Ni marufuku kwa mtu yeyote kuharibu miti, majani ndani ya uzio, kufunga nanga ya mitumbwi kwenye nguzo za uzio, kupita majini kwa miguu na kuchota au kuteka maji ndani ya eneo la mwalo

18. Ushuru katika eneo la Mwalo utatozwa na Halmashauri ya Manispaa kwa taratibu zilizowekwa na Sheria Ndogo za Halmashauri

19. Magari yote yatakayobeba samaki yatakuwa magari maalum yenye cheti cha samaki kutoka Afisa Mfawidhi wa udhibiti wa ubora wa samaki na viwango.

20. Magari yote maalum yatapaswa kuwa na nembo ya samaki ubavuni na picha ya samaki.

21. Magari hayo yasiwe na vumbi au kutu

22. Magari yawe na milango iliyotengenezwa kwa kutumia vifaa vinavyokubalika katika viwango vya ubora.

23. Ni kosa kwa mtu yeyote awe mvuvi muuzaji au mnunuzi wa samaki, mfanyakazi wa kiwanda cha samaki kutupa ovyo samaki wakati wa kupakua au kupakia samaki kwenye treyi, mabini au gati.

24. Ni marufuku kwa mtu yeyote awe mvuvi au agenti kununua samaki wenye mchanga au samaki walio kwenye sehemu chafu na maeneo yasiyorasmi.

25. Ni marufuku kwa mtu yeyote /mvuvi kuvua na kuuza samaki aina ya sangara walio chini ya urefu wa sentimeta 50 na samaki wa aina ya sato walio chini ya sentimeta 25.

26. Ni marufuku kununua au kuuza samaki mchanganyiko au kuchanganya pamoja aina tofauti za samaki.

27. Ni marufuku gari maalum ya kubebea samaki kuja kituoni ikiwa na barafu chafu kwa ajili ya kuhifadhia samaki ili wasiharibike.

28. Ni marufuku kwa agenti wa kiwanda kununua samaki waliokwishaharibika.

29. Ni marufuku kwa boti au mtumbwi wa kukusanyia au kununulia samaki kutumia kontena chafu, vifaa vichafu, kuwa na abiria tofauti na wafanyakazi walioajiriwa na mwenye boti au mtumbwi au kubeba mizigo mingine tofauti na samaki waliokusudiwa.

30. Ni marufuku samaki wa aina yoyote kuuziwa nje ya uzio wa kupokelea samaki

31. Ni marufuku kupima samaki kwa kutumia mzani ambao hauna nembo ya watu wa vipimo na mizani.

32. Ni marufuku kutumbulia samaki Mwaloni na kutupa utumbo na mabaki ya samaki ovyo kwenye eneo majini au nchi kavu.

33. Mtu yeyote atakayekaidi na kukiuka au kwenda kinyume na kifungu chochote cha sheria ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini ya shilingi za kitanzania isiyopungua laki mbili na isiyozidi milioni moja au kifungo jela cha miezi kumi na miwili au vyote kwa pamoja

Nembo ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa katika Kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kilichofanyika tarehe ……mwezi ……mwaka 2017 mbele ya:

……..
MH. PATRICK WILLIUM GUMBO
MSTAHIKI MEYA
HALMASHAURI YA MANISPAA
MUSOMA

…….
FIDELICA G. MYOVELLA
MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MANISPAA
MUSOMA

NAKUBALI,

TAREHE …..... ……
DODOMA **MH. GEORGE B. SIMBACHAWENE (Mb)**
WAZIRI WA NCHI – OR - TAMISEMI